**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MWONGOZO WA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO







**UMETOLEWA NA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**OKTOBA, 2021**

**Toleo la kwanza 2021**

## YALIYOMO


DIBAJI ........ 2

1.0 UTANGULIZI ........ 3

2.0 MALENGO YA MWONGOZO ........ 3

2.1 Lengo Kuu la Mwongozo ........ 3

2.2 Malengo Mahsusi ya Mwongozo ........ 3

3.0 UMUHIMU WA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO ........ 4

4.0 UTARATIBU WA UWEKAJI WA ALAMA ZA UTAMBUZI ........ 4

4.1 Upatikanaji wa hereni na bei yake ........ 4

4.2 Aina ya Mifugo itakayowekwa alama za utambuzi ........ 4

5.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA UWEKAJI WA ALAMA ZA UTAMBUZI KWA MIFUGO ........ 5

5.1 Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo ........ 5

5.2 Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ........ 6

5.3 Ofisi za Kanda za Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (ZVCs) ........ 6

5.4 Majukumu ya Ofisi za Mikoa (Regional Secretariate) ........ 6

5.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 7

5.6 Majukumu ya Watoa Huduma Binafsi ........ 7

5.7 Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa ........ 8

5.8 Majukumu ya Mzalishaji na Msambazaji wa vifaa vya utambuzi ........ 8

5.9 Majukumu ya Chama cha Wafugaji Tanzania ........ 9

5.10 Majukumu ya Mfugaji ........ 9

6.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU ........ 10

7.0 HITIMISHO ........ 10

**DIBAJI**

Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo una manufaa mengi ambayo ni pamoja na: Kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, hakikisho la usalama wa chakula, kurahisisha biashara ya mifugo na mazao yake, udhibiti wa wizi wa mifugo na upatikanaji wa mifugo iliyopotea, kumbukumbu ya koosaafu za mifugo na kuwezesha wafugaji kupata mkopo na kuweka bima ya mifugo yao. Ili kutekeleza Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 na Kanuni zake za mwaka 2011, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kutambua na kusajili ng'ombe millioni 33.9, mbuzi millioni 24.5, kondoo millioni 8.5 na punda 657,389. Utambuzi wa mifugo hawa utafanyika kwa kutumia hereni za kielekroniki na usajili utafanyika kwenye mfumo maalum ambao utawezesha kuwa na kumbukumbu sahihi za aina, idadi ya mifugo, mtawanyiko wake nchini na taarifa nyingine muhimu zinazohusu mifugo.

Mwongozo huu umebainisha majukumu ya wadau mbalimbali wakiwemo Sekta ya Umma, Sekta binafsi, Chama cha wafugaji na Wafugaji. Majukumu hayo yatafanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo kwa lengo la kutambua na kusajili mifugo. Serikali itaingia makubaliano na sekta binafsi kwa ajili kusambaza na kuvisha mifugo hereni za kielentroniki kwa usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo wa uwekaji wa namba za utambuzi utaratibiwa na kusimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mwongozo huu unatoa bei elekezi ya hereni isiyozidi shilingi 1,750= kwa ng'ombe na punda na shilingi 1,000/= kwa mbuzi na kondoo.

Aidha, Mwongozo unaainisha utaratibu utakaotumika kuweka hereni kwa mifugo yote iliyokusudiwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Aidha, utekelezaji wake utachangia kuboresha huduma ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo.

Mwongozo huu umetolewa na Idara ya Huduma za Mifugo na utaanza kutumika rasmi tarehe 01/10/2021.

Prof. Hezron E. Nonga
**Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo**
**Oktoba, 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo linatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo ya mwaka 2010 na Kanuni zake za mwaka 2011. Utambuzi unaweza kuwa wa mnyama mmoja mmoja au wa kundi kwa maana ya alama moja kwa kundi la wanyama. Dhana ya Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo imeainishwa pia kwenye Mwongozo unaoitwa *Development of integrated multipurpose animal recording systems* (FAO 2016). Kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo, 2006, utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo ni nyenzo muhimu katika uzalishaji wenye tija na faida kwa mifugo na mazao yake katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Utaratibu huu unahusisha utambuzi, usajili na ukusanyaji wa takwimu za mifugo. Aidha, Ilani ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 imeielekeza Wizara kuimarisha utambuzi na usajili wa mifugo nchini ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wafugaji na mifugo yao.

Utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji ulianza mwaka 2014 mpaka 2017 ambapo ng'ombe zaidi ya milioni 17 walipigwa chapa na kanzidata ya TANLITS ilitumika kuweka kumbukumbu za utambuzi ili kuwezesha au kurahisisha ufuatiliaji wa mifugo (traceability). Upigaji chapa kwa ng'ombe uligubikwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na utunzaji hafifu wa kumbukumbu za mifugo iliyowekwa alama, kufutika kwa alama na kuharibu ubora wa ngozi kutokana na vidonda. Utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa njia ya chapa pia ulikwama kutokana na kukosekana kwa mfumo mzuri wa kitaifa, uduni wa miundombinu na vifaa vilivyotumika, upungufu wa wataalam na uelewa mdogo miongoni mwa wadau wa Sekta ya Mifugo.

Kati ya mwaka 2019 na 2020, Wizara ilianza utambuzi wa mifugo kwa njia ya kuweka hereni za kawaida hasa kwa ng'ombe wa maziwa, zoezi ambalo pia halikufanikiwa kutokana na changamoto ya bei kuwa kubwa. Mwaka 2021, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilibuni aina nyingine ya utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki (electronic eartags) ambazo taarifa za mifugo zitawekwa kwenye mfumo unaowezesha kupatikana kwa taarifa za mifugo kupitia vifaa mbalimbali vya mawasiliano ikiwa ni pamoja na simu janja.

## 2.0 MALENGO YA MWONGOZO

### 2.1 Lengo Kuu la Mwongozo

Mwongozo unalenga kuweka utaratibu mzuri wa kuwezesha Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo kwa kuonesha mahitaji, majukumu na wajibu wa kila mdau ili kufikia lengo la jumla la mifugo yote ya Tanzania kutambuliwa na kusajiliwa.

.

### 2.2 Malengo Mahsusi ya Mwongozo

(a) Kuainisha mzalishaji na msambazaji wa alama za utambuzi wa mifugo hususani hereni;

(b) Kuratibu usambazaji wa alama za utambuzi za kielektroniki ili kuwa na mtiririko mzuri wa namba za usajili;
(c) Kuwezesha ushiriki wa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo kwa faida ya wadau wote;
(d) Kuhakikisha kuwa ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda wanawekewa alama za utambuzi za kielektroniki na kusajiliwa kwenye mfumo;
(e) Kuhakikisha kuwa uwekaji wa alama za utambuzi za kielektroni kwenye mifugo unaambatana na ufuatiliaji wa mifugo inayouzwa, kufa au kubadilishwa umiliki;
(f) Kuandaa mfumo wa usajili wa mazingira ya mfugaji unaoonyesha jina la eneo, jina la mfugaji, sehemu (coordinates), mawasiliano, aina ya ufugaji, na tarehe za usajili wa mara ya kwanza.

## 3.0 UMUHIMU WA UTAMBUZI, USAJILI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO

Umuhimu wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ni pamoja na:

(i) Mifugo kutambulika ilipo na umiliki wake;
(ii) Kukabili magonjwa ya mlipuko;
(iii) Kuwa na hakikisho la usalama wa chakula;
(iv) Kurahisisha biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi;
(v) Udhibiti wa wizi wa mifugo;
(vi) Kurahisisha upatikanaji wa mifugo iliyopotea;
(vii) Kurahisisha uboreshaji wa koosaafu za mifugo;
(viii) Utambuzi unawezesha urahisi wa upatikanaji wa mikopo na bima ya mifugo.

## 4.0 UTARATIBU WA UWEKAJI WA ALAMA ZA UTAMBUZI

### 4.1 Upatikanaji wa hereni na bei yake

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na sekta binafsi imehakikisha hereni bora za kielektroniki zinapatikana kwa wingi na kwa wakati hapa nchini. Hereni zote zitakazotumika kwenye zoezi hili zitazalishwa nchini na zitawekwa alama maalum ya kielektroniki (barcode) ambayo itaweza kusomwa kwa kutumia kifaa maalum. Hereni zilizozalishwa zitasambazawa kwa Halmashauri au makampuni ya sekta binafsi yatakayokidhi vigezo vya kutoa huduma ya kuweka hereni kwenye mifugo. Bei elekezi ya kuweka hereni haitazidi shilingi 1,750= kwa ng'ombe na punda na shilingi 1,000/= kwa mbuzi na kondoo. Bei hizi zitatumika katika Halmashauri zote Tanzania Bara.

### 4.2 Aina ya Mifugo itakayowekwa alama za utambuzi

Mifugo itakayowekwa alama za utambuzi hususan hereni za kielectroniki iko katika makundi yafuatayo:

(i) Ng'ombe, punda, kondoo na mbuzi wenye umri wa zaidi ya miezi 3 wanaofugwa kwenye mashamba ya Serikali, Ranchi, mashamba ya watu binafsi na mifugo iliyopo kwenye maeneo yote ya unenepeshaji (feedlot);

(ii) Ng’ombe, punda, kondoo na mbuzi wenye umri zaidi ya miezi 3 wanaofugwa ndani (zero grazing);
(iii) Ng’ombe, punda, kondoo na mbuzi wenye umri zaidi ya miezi 3 wanaofugwa katika mfumo huria (extensive grazing);
(iv) Ng’ombe, punda, kondoo na mbuzi waliopelekwa minadani bila ya kuwa wamewekewa hereni za utambuzi;
(v) Ng’ombe, punda, kondoo na mbuzi wanaosafirishwa kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine kwa lengo la kuhama au wanaopelekwa machinjioni bila ya kuwa wamewekewa hereni za utambuzi;
(vi) Ng’ombe, punda, kondoo na mbuzi wanaoingizwa nchini au wanaosafirishwa kwenda nchi za nje bila ya kuwa wamewekewa hereni za utambuzi;
(vii) Ng’ombe, punda, kondoo na mbuzi wote wanaokuwa wanashikiliwa kwenye hifadhi za maliasili, mashamba au sehemu zingine baada ya kuhusika kwenye kuvunja Sheria na ikatokea walikuwa hawajawekwa hereni za utambuzi.

Ili kudhibiti utoroshaji au mwingiliano wa mifugo ya Tanzania na wale wa nchi zingine, hereni za utambuzi wa mifugo iliyoko kwenye Halmashauri za Wilaya katika maeneo ya mipakani utafanyika kwa hereni za rangi tofauti na za maeneo mengine. Hii pia itawezesha kugundua mifugo inayotoka maeneo mengine na kuja mipakani kwa lengo la kutoroshwa kwenda nje ya nchi. Mifugo yote iliyoko kwenye Hifadhi ya Ngorongoro pia itawekwa hereni za rangi tofauti ili kuweza kuitofautisha na mifugo mingine itakayoingizwa ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kinyume na Sheria;

## 5.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA UWEKAJI WA ALAMA ZA UTAMBUZI KWA MIFUGO

### 5.1 Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo

(i) Kuratibu na kuhakikisha upatikanaji wa njia bora za utambuzi wa kielektroniki zinazotambulika kisheria na kusambazwa kuwafikia wadau wote kwa wakati;
(ii) Kukusanya taarifa za uwekaji wa hereni za utambuzi kutoka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Authorities) kulingana na matakwa ya mfumo yanavyoelekeza;
(iii) Kuhakikisha zoezi la utambuzi wa mifugo unafanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo. Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo Sura 184 (Sheria Namba 12 ya Mwaka 2010) na Kanuni zake (GN No: 362 ya Oktoba 2011);
(iv) Kuhakikisha kuwa kuna usimamizi madhubuti kufikia malengo kusudiwa ya utambuzi na idadi yote wa mifugo iliyopo;
(v) Kusimamia ujenzi wa Kanzidata ya Mfumo wa Kitaifa wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo (Tanzania National Livestock Identification and Traceability System) ambao ulianza mwaka 2012;
(vi) Kuratibu uhamasishaji na ufuatiliaji wa zoezi zima la uwekaji alama, kuhakikisha wafugaji wamehamasishwa na kuelewa umuhimu wa utambuzi wa mifugo;
(vii) Kusimamia na kufuatilia namba na idadi ya hereni kwa kila Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(viii) Kuratibu zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji na kuhakikisha ngo'mbe, punda, mbuzi na kondoo wote nchini wanawekwa alama za utambuzi na kusajiliwa kwenye mfumo.

## 5.2 Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI

(i) Kuwa kiungo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Tawala za Mikoa katika kufanikisha utekelezaji wa maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu uwekaji wa hereni kwenye mifugo iliyopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni zinazohusiana na Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo;
(iii) Kutoa ushauri na uhamasishaji wa utambuzi wa mifugo katika Mikoa;
(iv) Kuratibu, kushauri, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa zoezi la utambuzi wa mifugo;

## 5.3 Ofisi za Kanda za Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (ZVCs)

(i) Kuhamasisha na kufuatilia zoezi la utambuzi linavyoendelea kwenye Halmashauri kwa kushirikiana na Sekta binafsi na Chama cha Wafugaji Tanzania;
(ii) Kukusanya taarifa za idadi ya mifugo iliyowekwa alama za utambuzi kwenye mfumo kila siku na kuziwasilisha wizarani kwenye dawati la utambuzi wa mifugo;
(iii) Kuhakikisha kuwa huduma ya utambuzi wa mifugo zinawafikia wafugaji wote kwenye Halmashauri zote katika Kanda husika na mifugo yao yote inawekwa alama za utambuzi na kusajiliwa;
(iv) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2010.

## 5.4 Majukumu ya Ofisi za Mikoa (Regional Secretariate)

Mamlaka za Mikoa zitakuwa na jukumu la kushiriki katika kuhakikisha zoezi la utambuzi wa mifugo linafanikiwa katika Halmashauri zote kwa:

(i) Kuzisimamia Halmashauri zote za Mkoa na kuhakikisha mifugo yote kusudiwa inatambuliwa na kusajiliwa;
(ii) Kushiriki katika kutoa elimu na kuhamasisha wadau; wafugaji, wafanyabiashara kwa kushirikiana na Wizara, Chama cha Wafugaji, Halmashauri kuhusu umuhimu wa zoezi la utambuzi wa mifugo;
(iii) Kushauri kuhusu namna bora ya zoezi la utambuzi wa mifugo wakati wowote ili kufanikisha zoezi;
(iv) Kuhakikisha vifaa vya utambuzi vinafika katika Halmashauri kwa wakati;
(v) Kuwa kiungo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, OR-TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika usimamizi, utekelezaji na ufuatiliaji wa kampeni ya kuweka alama za utambuzi na usajili wa mifugo.

### 5.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ni wajibu wa Mkurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo ya mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na wajibu kama ifuatavyo:

(i) Kuingia mikataba na mzalishaji na msambazaji wa hereni za utambuzi wa mifugo kwa njia za kielektroniki ili kuwa na utaratibu mzuri wa malipo;
(ii) Kuingia mikataba na watoa huduma wa makampuni binafsi za kuweka alama za utambuzi na kusajili kwenye mfumo wa mifugo kwa mjibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;
(iii) Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia Afisa Mifugo wa Wilaya, Afisa Utambuzi na Afisa TEHAMA atafuatilia na kuhakikisha kila mfugaji anafikiwa na huduma ya elimu stahiki, mifugo yake inawekwa alama za utambuzi na kusajiliwa kwenye mfumo;
(iv) Kutoa taarifa ya idadi ya mifugo iliyopo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Wizara ili kujua mahitaji ya hereni;
(v) Kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo;
(vi) Kuhamasisha wadau wa mifugo kutambua mifugo yao kwa kutumia njia za utambuzi zinatambuliwa na Serikali;
(vii) Kuhakikisha taarifa zote za utambuzi za kila siku zinaingizwa kwenye mfumo;
(viii) Kuhakikisha mifugo ikiuzwa minadani au kutolewa mahari taarifa za umiliki zinabadilishwa. Endapo mifugo itakufa au itachinjwa sharti iondolewe kwenye mfumo ndani ya wiki mbili (2) na mifugo inayozaliwa ikishafikisha umri wa miezi 3 itambuliwe na kusajiliwa kwenye mfumo;
(ix) Kila Halmashauri itakuwa na Afisa Utambuzi wa Mifugo aliyeteuliwa na shughuli yake kuu itakuwa ni kufuatilia mifugo inayouzwa, inayochinjwa na inayozaliwa na kununuliwa ili kuitoa na kuingiza kwenye mfumo;
(x) Kutunza vifaa vya uwekaji alama kwa mifugo kwa kila Kata ili kuwezesha uwekaji wa alama za utambuzi na usajili kuwa endelevu;
(xi) Vibali vyote vya kusafirisha mifugo ndani na nje ya nchi vitatolewa tu kwa mifugo iliyowekwa alama za utambuzi;
(xii) Kukusanya fedha za malipo na kutoa resiti za kielekroniki kwa wafugaji wanaopewa huduma za utambuzi wa mifugo yao;
(xiii) Kuhakikisha malipo ya fedha zote za hereni yanafanyika kabla ya mzalishaji na msambazaji wa hereni hajazipeleka kwenye Halmashauri husika kulingana na mahitaji ya wakati huo;
(xiv) Kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa zoezi la utambuzi wa mifugo na kuhakikisha taarifa zote zinahifadhiwa kwenye mfumo.

### 5.6 Majukumu ya Watoa Huduma Binafsi

(i) Kuhakikisha kuwa wamekidhi matakwa ya kisheria na kitaaluma ya utoaji wa huduma za afya za wanyama ikiwemo ya uwekaji wa alama za utambuzi kwa mifugo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Veterinari ya mwaka 2003 kwa

kuwa wamesajiliwa (Animal Health Services Company) na Baraza la Vaterinari la Tanzania (VCT);

(ii) Kuwasilisha maombi ya kazi ya kuweka hereni za kielektroniki katika mifugo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na pale atakapokubaliwa watawekeana mkataba wa kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji ya mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011;

(iii) Atatumia alama za utambuzi hususan hereni za kielekroniki zinazotambuliwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;

(iv) Kuingia makubaliano na Mamlaka za Serikali za Mitaa namna ya kuweka alama za utambuzi na kusajili mifugo kwa mjibu wa Sheria na Kanuni na, utaratibu wa malipo;

(v) Kushiriki katika maandalizi ya awali ya uwekaji wa alama za utambuzi yatakayoshirikisha vikao baina ya Halmashauri, Chama cha wafugaji na wadau wengine;

(vi) Kushirikiana na Chama cha Wafugaji katika eneo husika katika uhamasishaji na ufuatiliaji wa ufanisi katika utoaji wa huduma ya uwekaji wa alama za utambuzi wa mifugo;

(vii) Kutumia alama za utambuzi hususan hereni za kielektroniki zinazotambuliwa na Serikali;

(viii) Makampuni yaliyopata kazi ya kuweka hereni za kielektroniki kwa mifugo kuhakikisha yanafuata taratibu zote zilizowekwa na Wizara ya Mifugo kuhusu uwekaji wa hereni za kielektroniki kwa mifugo.

## 5.7 Majukumu ya Serikali ya Kijiji au Mtaa

(i) Kushirikiana na vyama vya wafugaji na viongozi wa mitaa kuhamasisha umuhimu wa alama za utambuzi wa wafugaji yote na kuhakikisha kila mfugaji anashiriki kikamilifu kwenye zoezi hili;

(ii) Kuandaa maeneo na miundombinu ya kutolea huduma ya utambuzi kwa mifugo;

(iii) Kuhakikisha mifugo yote kwenye Kijiji au Mtaa inawekwa alama za utambuzi;

(iv) Kutunza kumbukumbu za wafugaji ambao mifugo yao imetambuliwa na kusajiliwa na hiyo ndiyo itakuwa mifugo halali katika kijiji husika;

(v) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji, Mtaa au Wilaya pale ambapo kutakuwa na taarifa ya kuuzwa kwa mifugo, kutolewa mahari, kusafirishwa au kuchinjwa na;

(vi) Kutoa taarifa kwa Afisa Mifugo wa Kata, Kijiji, Mtaa au Wilaya pale inapotokea baadhi ya wafugaji wamekaidi kuweka alama za utambuzi kwa mifugo yao ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

## 5.8 Majukumu ya Mzalishaji na Msambazaji wa vifaa vya utambuzi

Mzalishaji na msambazaji ni mdau toka Sekta Binafsi aliyetambuliwa na kusajiliwa na Wizara kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza vifaa vya utambuzi wa mifugo Tanzania Bara. Ili kuwa na udhibiti kwenye kutoa namba za utambuzi, idadi ya hereni za utambuzi zinazozalishwa pamoja na kudhibiti ubora, Wizara imetoa zabuni kwa

Mzalishaji mmoja tu ambaye amepewa alama maalum ya kielektroniki (barcode) inayowekwa kwenye hereni za utambuzi. Hereni za utambuzi zitazalishwa hapa nchini na kusambazwa kwenya Halmashauri kwa utaratibu unaoratibiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Majukumu ya Mzalishaji na Msambazaji wa vifaa vya utambuzi ni pamoja na:

(i) Kuhakikisha kuwa amekidhi matakwa ya kisheria na kitaaluma ya uzalishaji na usambazaji wa vifaa vya utambuzi wa mifugo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Veterinari ya 2003 pamoja na kuwa wamesajiliwa na Baraza la Vaterinari la Tanzania;
(ii) Kuwa na kibali cha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufanya kazi hiyo;
(iii) Kuomba ya kazi (tender) ya kusambaza vifaa vya utambuzi wa mifugo kwa Mkurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwekeana mkataba wa kusambaza vifaa hivyo;
(iv) Kutengeneza na kusambaza vifaa vya utambuzi wa mifugo vya kutosheleza mahitaji na vyenye ubora stahiki kwa wakati na kwa idadi inayotakiwa;
(v) Kuzalisha vifaa vya utambuzi (hereni za kielekroniki) kulingana na mahitaji yaliyopo kutoka kwenye Halmashauri. Mzalishaji na Msambazaji hataruhusiwa kuzalisha hereni za kielektroniki zenye barcode ya Serikali na kuziuza kwenye maduka ya pembejeo za mifugo au kwingineko;
(vi) Kuuza vifaa vya utambuzi wa mifugo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa au kwa watoa huduma za mifugo binafsi waliokidhi vigezo na ambao wataenda kuziweka kwa mifugo na sio kuziuza madukani;
(vii) Kuwasilisha kwa Wizara nakala ya orodha na namba ya vifaa vya utambuzi vinavyosambazwa ili kuhakikisha kunakuwa na takwimu sahihi kwa kila Halmashauri iliyopelekewa vifaa hivyo;
(viii) Kulipia gharama za usambazaji wa vifaa vya utambuzi wa mifugo katika ngazi ya makao makuu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 5.9 Majukumu ya Chama cha Wafugaji Tanzania

(i) Kuhamasisha nchi nzima wafugaji kujitokeza kwa ajili ya kuweka alama za utambuzi wa mifugo yao yote;
(ii) Chama cha Wafugaji kuwezesha viongozi wa chama kuzunguka nchi nzima kuhamasisha zoezi la uwekaji wa alama za utambuzi;
(iii) Kuwahamasisha na kuwaelimisha viongozi wa wafugaji, wazee maarufu na wazee wa mila wa vijiji kutambua na kukubali zoezi la utambuzi wa mifugo na hatimaye kuwahamasisha kwa wafugaji wengine**.**

## 5.10 Majukumu ya Mfugaji

(i) Kuhakikisha kuwa ng’ombe, punda, mbuzi na kondoo wote anaowamiliki wamewekwa alama za utambuzi na wamesajiliwa kwenye mfumo na mtaalamu wa mifugo kutoka kwenye kijiji, Kata, Halmashauri au kampuni binafsi ya kutoa huduma za mifugo iliyopewa kazi hiyo na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kushirikiana na viongozi wa chama cha wafugaji katika Kijiji au Mtaa, Kata na Wilaya katika shughuli zote zinazohusu uwekaji wa alama za utambuzi;

(iii) Kupeleka kwenye vituo vilivyoainishwa na kuhakikisha mifugo yake yote imewekwa alama za utambuzi za kielektroniki na inatambuliwa;
(iv) Kulipia gharama za kuvalisha hereni mifugo yote kwa bei elekezi isiyozidi shilingi 1,750/= kwa ng'ombe na punda na shilingi 1,000/= kwa mbuzi na kondoo;
(v) Kutoa taarifa ya mifugo ndani ya siku 14 kwa Afisa mifugo wa Kijiji au Kata kuhusu mifugo iliyokufa, iliyochinjwa, iliyouzwa, iliyonunuliwa na iliyotolewa mahari ili iweze kuondolewa au kuingizwa kwenye mfumo wa usajili;
(vi) Kutoa taarifa ya mifugo iliyopoteza hereni za utambuzi ndani ya siku 14 kwa Afisa mifugo wa kijiji au Kata ili kupatiwa hereni nyingine za utambuzi na kusajiliwa kwenye mfumo na;
(vii) Kutunza daftari la kumbukumbu ya namba za hereni za utambuzi zilizowekwa katika mifugo yake kwa lengo la kutunza taarifa za umiliki.

## 6.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo utaanza kutumika rasmi tarehe 01/10/2021. Hivyo, mdau yeyote atakayekuwa kinyume na mwongozo huu katika kutekeleza majukumu ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.

## 7.0 HITIMISHO

(i) Mifugo yote ambayo haijatambuliwa (Ng'ombe, punda, kondoo na mbuzi) hawataruhusiwa kuuzwa minadani, kusafirishwa, kutolewa mahari au kuchinjwa machinjioni;
(ii) Mfugaji ambaye atakuwa hajaweka alama za utambuzi wa mifugo ataelimishwa zaidi na ifikapo mwezi Agosti 2022 atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria**;**
(iii) Zoezi la uwekaji alama za utambuzi na usajili liende sanjari na Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Chama Cha Wafugaji kutengeneza mpango bora uboreshaji wa maeneo ya malisho na upatikanaji wa maji kwa mifugo maana idadi yake itakuwa inajulikana;
(iv) Mfugaji akishaitambua mifugo yake aelimishwe namna ya kuwekeza kwenye kuboresha koosafu na kupanga namna ya kupata malisho yatakayotosheleza mifugo yake kwa mwaka mzima.